MAKOI FOUNDATION
"Together for Better Tomorrows"

REPORT YA MAANDALIZI YA CHARITY YA IKWIRIRI



Mkoa :	**Pwani - Rufiji**
Kata :	**Ikwiriri**
Jina la kituo :	**IKWIRIRI CHILDREN HOME**
Tarehe ya Charity	**05 April 2025**

1. Utangulizi

Makoi Foundation ni tasasi isiyo ya Kiserikali yenye usajili namba ***ooNGO/R/7708***, Inayofanya kazi nchi nzima kwa lengo la kusaidia jamii ya Watanzania kupitia watu wenye uhitaji, hasa wale wanaoishi katika vituo vinavyotambuliwa na serikali.

Kama ilivo lengo kuu la taasisi hii siku ya tarehe 05.04.2025 Makoi foundation tulifanikiwa kukitembelea kituo cha **IKWIRIRI CHILDREN HOME** Kwa lengo la kutoa misaada mbalimbali, Charity hii ilihudhuliwa na watu zaidi ya 120 (Marafiki wa Makoi Foundation) kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dar es salaam na mikoa ya karibu.

2. Malengo ya Shughuli

2.1 Malengo makuu

- Kutoa mahitaji Muhimu ya kibinadamu katika kituo cha Ikwiriri Children Home

2.2 Malengo Mahususi

- Kutoa Elimu kuhusu utoaji hasa kwa jamii zenye uhitaji
- Kuitambulisha Taasisi kwa Wananchi

3. Utekelezaji wa Shughuli na Matokeo Yake

Na	Shughuli Zilizofanyika siku hiyo	Matokeo
1	Utambulisho	Wakati wa safari kutoka Posta kuelekea Ikwiriri watu walipata nafasi ya kujitambulisha, ili tuweze kujua ili kuangeza wigo mkubwa wa kufahamiana na kujua nani anafanya nini na yupo wapi (Connections)
2	Michezo na Burudani	Washiriki walipata nafasi za kushiriki michezo mbalimbali na watoto kama kucheza mziki, hii ilileta mshikamano mkubwa na kujenga mahusiano mazuri kati ya washiriki na watoto wa kwenye kituo.
3	Mijadala	Washiriki walipata nafasi ya kusikiliza mijadara ya mada iliyotolewa na mshiriki kutoka taasisi ya **I GO ABROAD**

4	Kutoa Salamu za Shukrani kwa walezi wa Kituo	Mkurugenzi wa Makoi Foundation aliwapa bahasha zenye salamu za shukrani kwa muda wao wa kuwalea watoto katika kituo hicho
5	Ugawaji wa Mahitaji kwenye kituo	Makoi foundation ilikabidhi mahitaji muhimu katika kituo Mahitaji hayo ni kama ifuatavyo, Earing Aid, Viti vya magurudumu mawili, kofia na glasses za wenye Albino, Midori kwa ajili ya wototo wenye usonji, Mahitaji ya shule, Mahitaji ya Chakula, Sabuni, Vitasa vya milango pamoja na mashuka kwa ajili ya kujifunika.

4. Changamoto

I. Changamoto ya Mvua iliyosababisha kuchelewa kwa ratiba hasa ya kuondoka St. Joseph
II. Watu kuchelewa kufika Vituoni
III. Kukosewa kwa baadhi ya vituo vya njiani kupelekea watu kupishana na gari.

5. Mafanikio

I. Tulifanikiwa kufanya Charity kwa tarehe iliyopangwa bila kikwazo chochote
I. Tulifanikiwa kufikia lengo la kukusanya kiasi ya shiringi Millioni 10 na kufanikiwa kukusanya Tsh. 10,815,200
II. Tulifanikiwa kutoa mahitaji muhimu katika kituo na kuwafikia watu Zaidi 40 waliopo kwenye kituo hiko

6. Maoni ya Washiriki wa Charity

I. Mapendekezo Chariti ijayo ifanyike mkoa wa Morogoro
I. Mapendekezo kuwepo na tukio la kuwaunganisha watu pamoja ili kubadilishana mawazo
II. Mapendekezo kuzingatia muda wa kuondoka uzingatiwe ili kufika kituoni kwa wakati
III. Mapendekezo ya kuendelea na ushirikiano
IV. Kutembelea maeneo mengi Zaidi hata mbali
V. Mapendekezo ya taasisi kujenga kituo cha kulea watoto na kujihusisha na matibabu ya wagonjwa
VI. Tuendelee kujitoa na kufikia malengo yanayowekwa kwa kila charity
VII. Pongezi wa Viongozi kwa maandalizi mazuri ya charity hii
VIII. Kutoa taarifa mapema juu ya changizo la kila mwaka katika taasisi ili waweze kuchangia.

7. Hitimisho

Ripoti fupi hii Imeandaliwa na Ofisi ya katibu Makoi Foundation.

8. Viambatanisho

I. Jumla ya Michango iliyokusanywa Charity
I. Riport ya fedha Ikwiriri
II. Mahudhulio ya Charity ya Ikwiriri